**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAISI - TAMISEMI.**

**SHULE YA SEKONDARI MYULA,**
**S.L.P 112,**
**NAMANYERE-NKASI.**
**TAREHE......./......./20.....**

*Jina la Mwanafunzi*..............................................
..............................................................
*SHULE*.......................................................

## MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MYULA.

### 1.0 UTANGULIZI.

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari MYULA mwaka **2020**. Shule ya sekondari MYULA ipo umbali wa kilometa 51 kutoka halmashauri NAMANYERE mjini na kilometa 35 kutoka mkoani SUMBAWANGA. Aidha shule hii ipo katika kijiji cha Myula kata ya Myula Wilaya ya Nkasi (Namanyere) Mkoa wa Rukwa (Sumbawanga). Muhula wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021**, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021**, hivyo baada ya siku saba**(7)** unatakiwa uwe umeripoti shuleni vinginevyo nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi wa akiba.

### 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

**A. MAHITAJI KWAAJILI YA USAJILI.**

**(i) Aje na nakala moja ya cheti cha kuzaliwa.**

**(ii) Aje na fomu ya daktari iliyojazwa.**

**(iii)Aje na fomu ya mkataba wa mzazi/ mlezi na mwanafunzi (mtoto) iliyojazwa.**

**B. SARE YA SHULE**

**(i) WAVULANA:**

**Suruali**: Anatakiwa awe na suruali mbili (02) rangi ya Zambarau na Orenji. Mshono wa suruali: iwe na mifuko mitatu mmoja nyuma upande wa kulia na miwili pande zote kulia na kushoto pembeni na sio kubandika, iwe na rinda mbili kila upande na upindo wa chini (miguuni) ugeuzwe juu (turnup). Upana miguuni uwe wa **inchi 16** isiwe ya kubana. Suruali za mitumba na jinsi haziruhusiwi hapa shuleni.

**Shati**: Awe na mashati mawili (02) meupe (white) yenye mikono mifupi (short sleeve)

**Viatu**: Awe na viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa na kamba, na soksi rangi nyeupe, visiwe na sori ndefu na visivyo chongoka mbele.

**Sweta**: Awe na sweta rangi yaZambarau yenye shingo "V" kwa ajili ya kujikinga na baridi.

**Sare za michezo**:Awe na T-Shirt ya bluu na Tracksuit rangi ya bluu bahari na raba za michezo.

**Nywele**: Nywele ziwe fupi muda wote.

**(ii) WASICHANA:**

**Sketi**: Anatakiwa awe na sketi mbili (02) Zambarau na Orenji, mshono wa sketi ziwe na rindabox kubwa mbelena nyuma na rinda dogondogo nne kulia na nne kushoto yenye belti ndogo. **NB:** Sketi ziwe ndefu zifike kwenye viatu, sketi fupi haziitajiki. Hivyo mzazi unatakiwa kumshonea binti sketi ndefu ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.

**Shati**: Awe na mashati mawili (02) meupe(white) yenye mikono mifupi (short sleeves).

**Viatu**: Awe na viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa na kamba na soksi nyeupe, visiwe na sori ndefu na visivyo chongoka mbele.

**Sweta**: Awe na sweta rangi ya Zambarau lenye shingo ya "V" kwa ajili ya kujikinga na baridi.

**Sare ya michezo**: Awe naT-Shirt, Tracksuit rangi ya bluu bahari na raba kwa ajili ya michezo.

**C. VIFAA VYA MASOMO:**

(a) Daftari kubwa zisizopungua 12 (counter book)
(b) Mathematical set (mkebe) 1
(c) Aje na kamusi (Dictionary) moja ya kiingereza na Kiswahili.
(d) Aje na kalamu za kutosha, rula na penseli.

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu **Na.25** ya mwaka **1978** na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria **Na.10** ya mwaka **1995.** Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi,wazazi, wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii yote kwa ujumla ni jambo lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiy wakati wote.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na
(i) Kutunza mali ya umma.

### 3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE.

(a) Wizi
(b) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
(c) Kugoma na kuhamasisha mgomo
(d) Kutoa lugha chafu kwa mwanafunzi mwenzako, mwalimu,mlezi na jamii nzima kwa ujumla.
(e) Kupigana na mwanafunzi mwenzio, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.
(f) Kusuka mtindo usiotakiwa, wanafunzi wanatakiwa kuwa na nywele fupi muda wote wawapo shuleni.
(g) Kufuga ndevu
(h) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevywa
(i) Uvutaji wa sigara.
(j) Uasherati, mausiano ya jinsia moja, kuoa au kuolewa.
(k) Kupata ujauzito au kutoa Mimba.
(l) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za Nchi.
(m) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
(n) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(o) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkonon.
(p) Kudharau bendera ya Taifa.
(q) Kufanya jaribio lolote lile la kujiua,au kutishia kujiua kama vile kunywa sumu nk.
(r) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. FOMU YA MKATABA WA MWANAFUNZI KUTOSHIRIKI MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI SHULENI.**

Mimi ................................................mtoto wa ....................................................wa kijiji cha ..................................

Ninaapa kuwa nitasoma kwa bidii hadi kuhitimu kidato cha nne, sitaacha shule, sitashiriki mgomo wowote, fujo yoyote shuleni, sitaharibu Mali ya shule kwa makusudi na wala sitajihusisha na makosa ya jinai. Endapo nitafanya moja kati ya mambo hayo juu, hatua Kali za kisheria zichululiwe dhidi yangu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule au jela.

Sahihi....................................  Tarehe.........................

***(Fomu hii ijazwe na irudishwe shuleni)***

**5. FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO YA SHULE HII.**

Mimi...................................................mzazi/mleziwa ................................ mkazi wa kijiji cha .............................

ninakiri na kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yote yatolewayo na shule hii. Pia nitampatia mahitaji ya lazima mwanangu ili asome amalize shule kidato cha nne kwa kuhakikisha haachi shule kabla ya muda huo wa kumaliza masomo yake. Niko tayari nichukuliwe hatua Kali za kisheria iwapo mtoto wangu ataacha au atatoroka shule ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

Sahihi........................................  Tarehe..............................

**(Fomu hii ijazwe na irudishwe shuleni.)**

***NB: Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu***

*KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.*

*ELIA .K. ELIA*

*MKUU WA SHULE*

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MYULA
NKASI.

MYULA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 112,
NAMANYERE-NKASI.

**MEDICAL OFFICER**

...........................................

...........................................

**RE: MEDICAL EXAMINATION:**

MR/MISS:................................................

Please examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following categories.

1. Hemoglobin..............................................................................
2. P.V. Bleeding...........................................................................
3. Sight.......................................................................................
4. Blood pressure.........................................................................
5. Urine for Sugar and pregnancy.....................................................
6. Stool for routine examination......................................................
7. Asthma...................................................................................
8. Skin diseases...........................................................................
9. Leprosy...................................................................................
10. Pulmonary tuberculosis............................................................
11. Neurosis................................................................................
12. Venereal diseases....................................................................
13. Other serious diseases..............................................................

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical officer)

1. I have examined the above named student and consider that He/She is physically fit/ Unfit and mentally fit/ Unfit and mentally fit/ unfit for a full schooling.
2. Other comments..............................................................................................
   ..................................................................................................................
   ............................................................
   DATE........................................

...................................................

SIGNATURE AND OFFICIAL STAMP

**NB:** ***NENDA HOSPITALI NA FOMU HII KWA AJILI YA VIPIMO KISHA IRUDISHE SHULENI.***